# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSIANA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS,
KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika: Kwanza kabisa, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu kwa kutujaalia uzima na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Kumi, Mkutano wa Saba kwa ajili ya kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi. Aidha, ninakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika na Wasaidizi wako kwa kuliongoza Baraza hili kwa ufanisi mkubwa. Imani yangu ni kwamba mtaendelea kuliongoza Baraza hili kwaweledi na uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika: Aidha, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu na kuhakikisha kuwa maendeleo makubwa yanapatikana pamoja na kuendelea kuidumisha hidaya ya Wazanzibari ambayo ni amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu inampongeza Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa

Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake hasa ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uadilifu na ueledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika: Sambamba na hayo, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Harous Said Suleiman kwa uteuzi alioupata hivi karibuni kuwa Waziri wa Wizara hii, pamoja na kuwashukuru watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hii Dkt. Omar Dadi Shajak bila ya kuwasahau watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mashirikiano yao waliyoyaonyesha wakati wa kupitia makadirio ya Bajeti ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika: Aidha, nitumie nafasi kuendelea kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu na kuhakikisha kuwa thamani halisi ya fedha inapatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa kila Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika: Kwa heshima na taadhima, naomba sasa kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu, na |

*9.* Ndg. Amina Abeid Hemed Mkalimani

Mheshimiwa Spika: Baada ya utangulizi huo sasa naomba nichukue fursa hii adhimu kutekeleza jukumu langu la msingi la kutoa maoni ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa mbele ya Baraza lako Tukufu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa mafungu yote yaliyochini ya Wizara hii.

FUNGU B 01: OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS

Mheshimiwa Spika: Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, katika kipindi cha mwaka wa fedha *2022/2023* inategemea kutekeleza Programu kuu *tatu (3)* ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Mazingira, Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi, Programu ya Watu wenye Ulemavu na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Maelezo ya kina ya programu hizo yametolewa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri pamoja kitabu cha Bajeti cha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha cha mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika: Katika kupambana na mabadiliko ya Tabianchi visiwani Zanzibar na ili athari za mabadiliko ya Tabianchi ziweze kupungua katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, hatunabudi kutumia vyema rasiliamali zilizopo ili kuwa msaada bora katika mapambano haya. Ni jukumu la kila mmoja kufahamu kwamba athari za mabadiliko ya Tabianchi zinamuathiri kila mmoja na yapo maeneo ambayo tayari athari zake zinaonekana moja kwa moja na shughuli za kimaendeleo kushindwa kufanyika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika: Katika programu ya Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Mazingira imepangiwa Tsh. Bilioni 6.255 ambazo msingi wake ni kupambana na athari hizi katika nchi yetu, Kamati yangu inashauri Serikali kusimamia fedha hizi ili zipatikane kwa wakati na zitumike kama malengo yalivyopangwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii juu ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, mikakati maalumu

ianzishwe ya kusimamia upandaji wa miti na kulinda vyanzo vya maji kwa lengo la kurejesha uoto wa asili katika maeneo mbali mbali.

Mheshimiwa Spika: Kamati yangu pia, inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuratibu vyema programu ya Masuala ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar kwa namna inavyopambana na kupunguza unyanyasaji wa watu wenye ulemavu katika jamii. Aidha, Kamati pia inaishukuru Taasisi hii kwa kuwa na huduma ya Kukuza Upatikanaji wa Haki na Fursa kwa Watu wenye Ulemavu, huduma ambayo itawasaidia wenzetu hawa kupata haki zao za msingi lakini pia fursa kama ilivyo kwa watu wengine. Aidha, kwa nafasi hii napenda nitoe wito kwa wananchi wote kuwashirikisha kikamilifu watu wenye ulemavu katika zoezi la Sensa linalotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika: Kupitia programu hii, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kukuza uelewa kwa jamii juu ya Watu wenye Ulemavu ni kiasi cha Tsh. Miloni 35.15 ambayo kidogo mno na hazikidhi mahitaji, kama kweli tuna lengo la kujenga uelewa kwa jamii juu ya masuala ya watu wenye ulemavu na pia hatutaweza kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hata hivyo, Kamati yangu inashauri fedha hizo zilizopangwa zipatikane na kwa wakati muafaka ili kutekeleza majukumu yao kwa wakati.

## FUNGU B 04: MAMLAKA YA UDHIBITI WA MAZINGIRA

Mheshimiwa Spika: Katika hali ambayo si ya kawaida na ya kusikitisha sana ni kuona haiba ya mazingira yetu ikipotea kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanywa kutokana na shughuli mbali mbali za kijamii na kiuchumi, jambo ambalo kila mmoja athari zake zinamfikia. Kutokana na hali hiyo, yapo maeneo mengi pembezoni mwa bahari yetu ya Zanzibar kama vile ukanda wa Jambiani na Paje ikiwa yamethirika sana na uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za kiuekezaji zinazofanyika kila siku.

Mheshimiwa Spika: Kupitia programu kuu ya Usimamizi wa Mazingira, Kamati inaiomba Ofisi kufanya utafiti wa kina wa kimazingira kwa maeneo yote yaliyoathirika na hatua za kimkakati kuchukuliwa kwa lengo la kunusuru maeneo hayo na mmong’onyoko wa ardhi

na hatimaye kupotea kwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika: Kamati yangu inaishauri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kukaa na wawekezaji wa Hoteli zilizopo katika ukanda huu ili kukubaliana namna ya kuyanusuru maeneo haya kwa kuanzisha ujenzi wa kuta ambazo zitafuata ushauri wa kitaalamu wa Idara ya Mazingira ili kunusuru maji ya chumvi kuingia katika makazi ya watu pamoja na kupotea kwa fukwe ambazo ndio kivutio kikubwa cha Utalii katika maeneo haya. Aidha, Kamati inatoa wito mamlaka zote zenye kusimamia mazingira Zanzibar kuhakikisha wanatoa elimu kwa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira pamoja na kuzifuatilia changamoto zote zinazoyakabili mazingira yetu. Sambamba na hilo, Kamati inaiomba Serikali kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mazingira Nam.3 ya Mwaka 2015 ambayo itasaidia utekelezaji wa kazi zao kuwa rahisi kabisa.

FUNGU C 04: MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Mheshimiwa Spika: Kupitia programu kuu ya Udhibiti wa dawa za kulevya; Kamati yangu inampongeza Kanali Burhan Zubeir Nassor kwa kuteuliwa kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar pamoja na kufanikiwa kutekeleza opresheni mbali mbali kwa vipindi tofauti ndani ya Mji wa Zanzibar na Vitongoji vyake na baadhi ya maeneo Kisiwani Pemba. Kamati inaamini operesheni hizi zikiendelea ambazo zinaongeza mapambano dhidi ya dawa za kulevya zitapunguza kwa kiasi kikubwa uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya katika jamii na hatimaye kupunguza kabisa athari za janga hili katika jamii yetu.

Mjeshimiwa Spika: Aidha, Kamati kwa kiasi Fulani imeridhishwa na nguvu ya mapambano kutokana na uwepo wa jumla ya kesi 51 zilizoripotiwa na kufanyiwa kazi katika ngazi mbali mbali za kisheria zikiwemo kesi 23 kwa DPP, kesi 17 kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na kesi 5 zimefunguliwa Mahakamani pamoja na kesi 6 ambazo zinaedendelea na upelelezi. Licha ya juhudi hizo, Kamati yangu inashauri Mamlaka kusimamia kikamilifu kesi hizo na kuhakikisha wameweka mbali muhali na kuonea

huruma katika kesi hizi ili adhabu kali itolewe kwa mujibu wa Sheria ya Dawa za Kulevya lakini pia kwa kuzingatia athari zinazopatikana katika jamii dhidi ya janga hili.

Mheshimiwa Spika: Ili Zanzibar iweze kufanikiwa katika mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya ni lazima kuongeza nguvu katika kuimarisha rasilimali fedha na rasilimali watu, vitu ambavyo ndio nyenzo muhimu katika mapambano na kufikia malengo. Hata hivyo, juhudi zote zinazofanyika haziwezi kutimia ikiwa fedha zinazoidhinishwa katika matumizi hazitopatikana na watendaji wakawezeshwa katika Nyanja mbali mbali.

Mheshimiwa Spika: katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka iliidhinishiwa kiasi cha Tsh Milioni 874.2 kwa matumizi mengiyo (OC) ambapo hadi kufikia mwezi wa March 2022 Mamlaka imeingiziwa Tsh Milioni 374.6 sawa na asilimia 43 kwa matumizi mengineyo. Kamati inasikitishwa na asilimia ndogo ambayo imetikana kwa kipindi cha miezi 9 ikihofia kwamba baadhi ya kazi kama vile operesheni za baharini na vijijini, kutoa elimu kwa umma na kuziendeleza nyumba maalumu kwa ajili ya waathirika wa dawa za kulevya (soba house) hazikuweza kufanyika kwa ufanisi kutokana na changamoto ya rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika: Kamati yangu inaishauri Serikali kupitia sheria mpya Nam 8 ya Mwaka 2021 ya Dawa za Kulevya kuhakikisha Mamlaka hii inapatiwa fedha za kutosha pamoja na wataalamu mbali mbali ambao ndio nyenzo kuu ya kujenga mapambano ya Dawa za Kulevya kwa lengo la kuimarisha utendaji wao ili kwenda sambamba na maadhimio ya kikanda na kimataifa.

FUNGU C 05: TUME YA UKIMWI

Mheshimiwa Spika: Fungu hili limepangiwa kutekeleza programu kuu mbili ambazo ni kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI na Uratibu wa Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI. Maelezo ya kina ya programu hizi tayari yameshatolewa ufafanuzi wa kina hapo awali.

Mheshimiwa Spika: Kamati yangu inashauri katika programu ndogo ya Mawasiliano na

Utetezi wa Masuala ya UKIMWI ambayo kwa mwaka unaokuja wa 2022/2023 imepangiwa kiasi cha Tsh. Milioni 82.4 kwa ajili ya shughuli za kutoa elimu ya UKIMWI na mabadiliko ya Tabia kwa jamii; fedha hizi ni ndogo ukilinganisha na fedha za mwaka huu unaomalizika ambao ilipangiwa Tsh Milioni 161.9 licha ya mabadiliko madogo ya programu yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika: Kamati yangu inapata wasi wasi kidogo kuona zoezi la utoaji wa elimu na mabadiliko ya tabia halitofanikiwa kikamilifu kutokana na kiasi kidogo cha fedha zilizopangwa. Hivyo basi, Kamati inashauri juhudi mahasusi zifanyike kwa lengo la kuiboresha programu hii katika rasilimali fedha na rasilimali watu pamoja na kupatiwa fedha zote ambazo zimepangwa ili kutekeleza malengo yake kwa wakati.

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika: Mwisho, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kufikiria kwa makini kuipatia fedha za kutosha Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar kwasababu waathirika wakubwa ni vijana, na vijana ndio msingi wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika: Mwisho kabisa, ili kufikiwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie, wairidhie Bajeti hii na hatimae waidhinishie Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais makadirio na makisio ya fedha zote zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ili waweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika: *kwa niaba ya Kamati yangu* *Naomba Kuunga Mkono Hoja.*

Ahsante,

…………….…………….

(Machano Othman Said)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR.